TANGAZO LA SERIKALI NA. 235 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MANHEIGAN YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Manheigan ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

*Tangazo la Serikali Na. 235 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 497825.418MS, 9621776.672KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ84º45'54.01''MG kwa umbali wa kilomita 1.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 509367.670MS, 9579816.839KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KZ29º04'48.44''MG kwa umbali wa kilomita 2.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 500349.700MS, 9619781.046KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi - Kusini katika uelekeo wa KZ32º11'00.87''MS kwa umbali wa kilomita 0.861 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 499891.066MS, 9619052.285KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS65º23'52.19''MS kwa umbali wa kilomita 2.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 497558.165MS, 9620120.478KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KS09º09'59.73''MG kwa umbali wa kilomita 1.68 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*